

**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA
UFUNDI STADI (NACTVET)**



**TAARIFA KWA UMMA
KUHUSU UDAHILI WA MUDA WA NYONGEZA KATIKA
PROGRAMMU MBALIMBALI KWA MKUPUO WA SEPTEMBER
2023/2024**

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linataarifu umma kuwa limefungua udahili wa muda wa nyongeza katika program mbalimbali kuanzia tarehe 17 hadi 20, Oktoba, 2023. Muda huu utatumika pia kwa ajili ya vyuo kurekebisha na kusahihisha kasoro zilizojitokeza na pia kuwasilisha wanafunzi waliosahaulika.

Hivyo, waombaji wanashauriwa kutuma maombi kwenye vyuo wanavyopenda kuanzia tarehe 17 hadi 20 Oktoba, 2023 na vyuo kufanya uchaguzi na kuwasilisha kwenye Baraza kwa ajili ya uhakiki. Waombaji waliochaguliwa watafanyiwa uhakiki kuanza tarehe 21 hadi 23 Oktoba, 2023 kwa ajili ya kuanza masomo.

Tunapenda kutoa rai kwa vyuo na waombaji kutumia muda huu kwa makini ili kuepuka usumbufu kwa wanafunzi wanaosajiliwa pasipo kuhakikiwa. Baraza halitasita kuchukua hatua stahiki kwa chuo kitakachokiuka taratibu za udahili kwa mwaka 2023/2024.

**IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI
STADI (NACTVET)**

17/10/2023